035713655

**KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS**

# KCPE

516004

# KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**

   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
   A. waraka
   B. barua maalum
   C. barua ya kiofisi
   D. Barua rasmi

   Jibu sahihi ni **D**

   **Katika karatasi ya majibu:**

   **2.** [A] [B] [C] [D] **12.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **32.** [A] [B] [C] [D] **42.** [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© *Mtihani Bora*

**GEUZA UKURASA**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Baada ya ___1___ kusikiliza na kuona kwamba ___2___ ulikuwa wa kuridhisha, alitoa hukumu yake mara moja. Alisema ___3___ mshtakiwa ___4___ na hatia ya kuiba kuku ___5___ jirani yake. ___6___ faini ya shilingi elfu mbili ama kifungo cha robo mwaka yaani miezi ___7___. Mwizi yule alijitetea na akaomba kusamehewa lakini ___8___. Madhali hakuwa na hela, alitolewa na kupelekwa ___9___ mara moja.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. korti | B. mahakama | C. hakimu | D. wakili |
| **2.** | A. ushahidi | B. ushuhuda | C. idhibati | D. makosa |
| **3.** | A. kuua | B. kua | C. kwa | D. kuwa |
| **4.** | A. atapatikana | B. alipatikana | C. angepatikana | D. anapatikana |
| **5.** | A. la | B. ya | C. za | D. wa |
| **6.** | A. Alitoleshwa | B. Alituzwa | C. Alitozwa | D. Alitoswa |
| **7.** | A. mitatu | B. minne | C. sita | D. miwili |
| **8.** | A. alipiga ubwete | B. hakufua dafu | C. alienda masia | D. hakula mwata |
| **9.** | A. kizimbani | B. rumande | C. korokoroni | D. jela |

Wahenga walisema kuwa ___10___. Barobaro yule ___11___ na kidosho mmoja aliyetoka mjini. ___12___ miaka miwili wapenzi hawa walikonda kama ___13___. Urembo uliokuwa umevutia barobaro yule ukabadilika na kuwa kero. Walienda hospitalini ili kujua ___14___ yaliyowanyima usingizi. Baada ya kutumwa ___15___, walijua kuwa walikuwa na Ukimwi. Mvulana yule alijuta kuvutiwa na urembo ule.

**10.** A. uzuri wa kuyu ndani mabuu
B. akumulikaye mchana usiku atakuchoma
C. aisifuye mvua jua imemnyea
D. mumunye huharibika ukubwani

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. alipata jiko | B. alifunga safari | C. aliasi ukapera | D. alienda mrama |
| **12.** | A. Badala ya | B. Kabla ya | C. Kwa kuwa | D. Baada ya |
| **13.** | A. ng'onda | B. unyoya | C. sindano | D. samaki |
| **14.** | A. ugonjwa | B. maradhi | C. ukongo | D. shida |
| **15.** | A. maktaba | B. wadi | C. maabara | D. leba |

***Katika swali la 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Kati ya sentensi hizi ni ipi inaonyesha masharti?
A. Mwezi huonekana saa moja jioni.
B. Ungemwona jana ungempa pesa zake
C. Ukiwa na bidii utapita mtihani
D. Alipohamia hakuna mtu anayejua

**17.** Ni nini udogo wa sentensi hii?
***Ndovu yule ana miguu mikubwa.***
A. Dovu lile lina guu kubwa
B. Kidovu kile kina miguu mikubwa
C. Madovu yale yana maguu makubwa
D. Kidovu kile kina viguu vikubwa

18. Chagua orodha yenye vielezi pekee.
A. Jana, vizuri, mwakani, polepole
B. Vibaya, virefu, mfupi, vigumu
C. Kisumu, mlango, mtoto, kiroboto
D. Huyu, yule, mimi, wao

19. Sayari ya pili kutoka Jua ni ipi?
A. Zaibaki B. Dunia
C. Zuhura D. Mirihi

20. Tegua kitendawili hiki.
***Likitoka halirudi.***
A. jino B. mwangwi
C. shoka D. neno

21. Chagua sentensi sahihi kisarufi.
A. Mtu mwenye ameenda tunamjua.
B. Angelinunua gari lile angefurahia
C. Tulikuwa tunatazama runinga leo
D. Ala? Kumbe Juma ni mwizi?

22. Ni maelezo yapi si sahihi?
A. Malenga huyaimba na kukariri mashairi
B. Kuli hufanya kazi ya kupakia mizigo
C. Mhasibu huweka rekodi za matumizi ya pesa.
D. Mhazigi hutibu viungo vya mwili vilivyovunjika.

23. Badili sentensi hii iwe katika ngeli ya PA- KU- MU.
***Uwanja wao una nyasi ndefu***
A. Uwanjani wao una nyasi ndefu
B. Uwanjani pao pana nyasi ndefu
C. Uwanjani wao mna nyasi ndefu
D. Uwanjani mwao kuna nyasi ndefu

24. Chagua sentensi iliyotumia kivumishi halisi.
A. Uji mwingi ulipikiwa watoto wadogo
B. Mbwa wale walibweka usiku mzima
C. Mashamba yenu yana mimea mingi
D. Wanafunzi wengine watatuzwa kesho

25. Tumia kiunganishi mwafaka kujaza pengo.
_____***utakapomwona mnyama kimbia.***
A. Punde B. Taraa
C. Mradi D. Aghalabu

26. Mjomba ni kwa halati kama vile fahali ni kwa
A. koo B. mbuzi
C. mtamba D. ng'ombe

27. Chagua sentensi inayoonyesha **kwa** ya **ala**
A. Alikunywa maji kwa bilauri
B. Wavulana kwa wasichana walicheza
C. Tulienda moja kwa moja hadi kwao
D. Kwa mjomba kuna mitunda mingi.

28. Mtu ambaye huongea kwa ncha ya ulimi huitwaje?
A. Kigugumizi B. Kinyonyoke
C. Kibogoyo D. Kithembe

29. $\frac{2}{7}$ kwa maneno ni
A. tusui saba B. nusu saba
C. thumni mbili D. subui mbili

30. Ni neno gani ambalo ni nomino kutokana na kitenzi **lia**?
A. Lilia B. Mlio
C. Liza D. Ulili

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31- 40</u>***

Alikuwa kwenye ulimwengu mwingine wa usingizi na ndoto zilizopumbaza hadi alipobumburushwa na sauti tamu na nyororo ya kike. Limbukeni aliyafungua macho yake mazito kwa shida, akanyosha mkono na kuyafikicha macho yake kwa bapa la mkono wa kulia. Aliweza kuyafungua macho polepole na kuiona sura ya mwanamke aliyeonekana kama kivuli kinachoelea majini. Aliutoa ulimi wake na kujilambalamba kujiamsha. Aliguna kidogo kama mtu asiyetaka kuamka. Aliona haya kuwa alikuwa amesimamiwa.

"Ndugu, amka! Kisha ukaze mkanda wako, ndege karibu inatua," yule mwanamke alimgutusha. Limbukeni alipambaukiwa na ukweli sasa. Safari yao ilikuwa imefikia hatua ya mwisho. Alikuwa na hamu kubwa ya kuwasili nyumbani na kujiunga na ndugu na <u>jamaa</u> zake ambao alitengana nao kwa muda ulioonekana sasa kama karne. Alifanya kama alivyoshauriwa. Alijitahidi kuivuta shingo yake karibu na dirisha dogo la ndege alimosafiria. Hakuweza kuona chochote. "Lazima ndege bado iko juu mawinguni," alijiambia.

Aliyaangaza macho yake na kuangalia sehemu alikokuwa ameweka mizigo yake. Alikuwa na kisanduku kidogo alichoweka sehemu ya mbele, karibu na miguu yake. Aliruhusiwa kukihifadhi hiki hapa. Mfuko mwingine mkubwa ulikuwa kwenye sehemu maalum ilikowekwa mizigo; sehemu ambazo zilikuwa zimefungwa imara zote. Limbukeni alikuwa na furaha kubwa kuwa hatimaye amefika nyumbani. Wasiwasi aliokuwa nao na hofu nyingi kuhusu safari za ndege vilishamyeyusha.

Yeyote aliyemtazama aliweza kumtambua kuwa alikuwa na furaha isiyo na kifani. Alitazama hapa na pale; uso ulimchanuka kama ua linalofumbuka. Karibu na mlango wa sehemu inayotenganisha wanakokaa abiria wa daraja la kwanza na alikokuwa yeye (abiria wa daraja la pili), palikuwa na mwanamume aliyeangalia huku na huku. Limbukeni alimwangalia mara kadha. Alishangaa ni kwa nini hakuonekana na furaha. "Hivi kwa nini? Hana raha ya kufika nyumbani? Hashukuru Mungu kwa kuwasili?"alijiuliza Limbukeni.

Mara mbili walipoyakutanisha macho yao, Limbukeni alivuta tabasamu. Yamkini angemsaidia kuliondoa wingu la wasiwasi lililomtanda usoni. Limbukeni alifanya hivi mara kadha. Hatimaye yule jamaa aliyevalia magwanda nadhifu kupindukia alitabasamu naye.

---

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, si kweli kusema kuwa
A. Limbukeni aliamshwa na mwanamke
B. Limbukeni hakupenda kulala na kuota
C. Limbukeni alikuwa na kasoro ya macho
D. Limbukeni aliguna na alikataa kuamka.

**32.** Unafikiri ni kwa nini Limbukeni aliona soni?
A. Kulala na kuota mambo mengi
B. Kuona angefika nyumbani salama
C. Kuangaliwa na abiria wenzake
D. Kusimamiwa na mhudumu wa ndege

**33.** Limbukeni alipoamka
A. ndege ilikuwa ikitia nanga
B. ndege ilikuwa imetulia uwanjani
C. ndege ilikuwa iking'oa nanga
D. ndege ilikuwa karibu na anga

**34.** Ni neno lipi halina maana sawa na **jamaa**?
A. Mbari B. Ndugu
C. Jamii D. Mlango

**35.** Ni kwa nini Limbukeni hakuona nje alipotazama?
A. Dirisha lile lilikuwa dogo sana.
B. Ndege ile aliyosafiria haikuwa imetua
C. Hakuwa karibu na mahali penye uwazi
D. Alikuwa na usingizi mwingi mno

**36.** Ni kweli kusema kuwa mizigo ya abiria
A. ilionekana yote mahali ilihifadhiwa
B. iliwekwa mahali ambapo hapakufungwa
C. yote ilihifadhiwa sehemu maalumu
D. haikuonekana yote mahali ilihifadhiwa

**37.** Kulingana na kifungu hiki
A. karne moja ilipita kabla ya Limbukeni kwenda kwao
B. Jamaa na marafiki walimngoja Limbukeni
C. ndugu za Limbukeni walikuwa wamemsahau
D. Limbukeni alikuwa ametengana na ndugu zake

**38.** Ni jambo gani lilionyesha kuwa Limbukeni alikuwa na hamu ya kufika nyumbani?
A. Kuzinduka usingizini
B. Kutazama dirisha dogo
C. Furaha aliyokuwa nayo
D. Kutabasamu na rubani

**39.** Ndege aliyosafiria Limbukeni na abiria ilikuwa
A. kubwa kuliko nyingine
B. ya matabaka tofauti
C. na madaraja mengi
D. na wanaume pekee

**40.** Ni bayana kuwa mwanamume aliyemwangalia Limbukeni
A. alikuwa na huzuni nyingi
B. hakupenda kushukuru Mungu
C. huenda hakuwa na furaha
D. alikuwa amekasirika sana

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41- 50.***

Mwanadamu heshi kuumbwa'. Naye heshi kuunda na kuvumbua kadiri anavyoumbwa. Kwa kutumia akili na werevu aliojaaliwa na Maulana, mwanadamu ameusoma ulimwengu, akausawiri na kuutafiti kiasi cha kuuboresha. Sasa anajigamba kwa kutumia sayansi na teknolojia ili kufidia mahitaji yake.

Maumbile yametufunza kuwa mtoto azaliwapo hutambaa kabla ya kusimama dede. Vivyo hivyo ndivyo hatua za uvumbuzi wa binadamu zilivyoanza. Kutambaa kwa maendeleo ya mja kulianza kwa matumizi ya jiwe kama kifaa cha kutendea kazi zote. Karne hizo za mawe zikapita na mapito yake yakawa historia.

Ulimwengu wa karne ya sasa ukaingia katika kipindi cha maendeleo ya hali ya juu ya uvumbuzi. Utafiti wa sayansi ukaboreka na teknolojia ikaongezeka. Teknolojia mbalimbali zikazalika, mawasiliano, wenyewe wakiita *teknohama*. Teknolojia hii imeleta uvumbuzi wa tarakilishi, matumizi ya wavuti, barua pepe, simu tamba na mambo mbalimbali ya kustaajabisha. Mambo hayo ndiyo yameufanya ulimwengu kuwa katika hali iitwayo utandawazi, wengine wakiita utandaridhi. Hii ni ile hali ambayo mawasiliano yamekuwa kwa wepesi mno hadi dunia ikawa ni kama kijiji kidogo.

Sayansi katika **zaraa** imeleta maajabu yake. Utashangaa kuona kuku asiye na haja ya jogoo lakini anataga mayai. Kisha mayai hayo huangua bila kuatamiwa. Chakula na dawa vinatosha kumfanya kuku atage mayai hayo. Kuku wanaofungwa kwa ajili ya mitambo mbalimbali zinatumiwa kurahisisha shughuli za kilimo. Isiwe ni ajabu kuona tingatinga moja likifanya kazi zote shambani. Tingatinga hilo litavuna nafaka, lichuje, litie kwenye magunia na hatimaye kushona magunia hayo. Kwa kutumia uvumbuzi wa sayansi, mwanadamu amemudu kuongeza mazao yake shambani na hata kuyaboresha. Utafiti umewezesha mimea, matunda na mboga kukua na kupevuka kwa muda mfupi.

**41.** Mwanadamu hutumia nini ili kuyafanya maisha yawe bora?
A. Sayansi ambayo ni bora.
B. Maarifa aliyopewa na Mungu
C. Teknolojia na majaaliwa ya Maulana
D. Maajabu ya Mungu ambayo ni adimu

**42.** Teknolojia na sayansi imewezaje kukimu mahitaji ya waja?
A. Kusawiri na kuboresha maisha ya wachache
B. Kuusoma ulimwengu na kukerwa na mawazo
C. Kufidia mahitaji na kuomba Maulana
D. Kulipia mambo ambayo binadamu anataka.

**43.** Hatua za uvumbuzi zinalinganishwa na nini?
A. Maisha ya mtoto mdogo
B. Maumbile ya mtoto
C. Kusimama kwa mtoto
D. Kuzaliwa kwa mtoto

**44.** **...kutambaa kwa maendeleo ya mja kulianza kwa matumizi ya jiwe kama kifaa cha kutenda kazi zote.** Ni methali gani inaafikiana na maelezo haya?
A. Kilichompata peku hata na ungo ni hicho
B. Mhini na mhiniwa njia zao ni moja
C. Haba na haba hujaza kibaba
D. Safari ndefu huanza kwa hatua moja

**45.** Ni mambo gani ambayo hayahusu teknolojia?
A. Kutuma barua kwa umeme
B. Kutumia wavuti na kompyuta
C. Kutumia selula na tarakilishi
D. Kutuma ujumbe kutumia tarakilishi

**46.** Dunia imekuwa kama kijiji kidogo kwani
A. kuwasiliana na kusafiri kwa wepesi
B. mawasiliano yamekuwa mepesi
C. utamaduni na usafiri mwema
D. kutangamana na watu wa dunia

**47.** Chagua kisawe cha neno **zaraa**.
A. ujira
B. biashara
C. kilimo
D. wanyama

**48.** Ajabu ni kuwa
A. jogoo huwa wanataga mayai
B. mayai mengi huwa na jogoo
C. mayai hutotolewa bila kuatamiwa
D. kuku wote hukua kwa wiki nne

**49.** Mazao yamekuwa mengi kwa kuwa
A. tingatinga hufanya kazi nyingi
B. sayansi imevumbua mambo mazuri
C. mwanadamu amenunua vifaa vingi
D. matunda hupevuka kwa muda mfupi

**50.** Kichwa mwafaka cha kifungu hiki ni
A. Kilimo na teknolojia
B. Ukulima na sayansi
C. Utafiti wa teknolojia
D. Uvumbuzi wa teknolojia